

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE



TAARIFA KWA UMMA

Gazeti la Mwananchi toleo namba 7959 la tarehe 24.06 2022 katika ukurasa wa barua za wasomaji liliandika **‘Wanafunzi Walemavu Katumba tunanyanyaswa’**

Baada ya taarifa hiyo viongozi ngazi ya wilaya walifuatilia kwa kina hii ikiwa ni pamoja na kuzungumza na Watumishi pamoja na Walimu wa shule hiyo na kubaini kuwa hakuna mwanafunzi yeyote anayenyanyaswa au kubaguliwa na kuwa aliyetoa taarifa hiyo alitoa kwa maslahi yake binafsi.

Katika kutoa taaluma na malezi uongozi wa shule hutoa huduma bila kubagua jinsia na hali ya Mwanafunzi kwa kufuata sheria, taratibu na kanuni za Serikali.

Kwa kutumia vikao vya shule wanafunzi wamekuwa wakitoa changamoto zao na kutatuliwa kwa wakati hii ikiwa ni pamoja na uongozi wa wilaya kufika kuwasikiliza wanafunzi, hao na kutoa misaada mbalimbali ya kibinadamu.

Aidha serikali katika kuhakikisha wanafunzi hao wanapata huduma bora ya elimu, malazi na chakula imejenga bweni lililogharamu jumla ya shilingi Million 80, Jengo la utawala Milloni 50, na vyumba vitano vya madarasa Million 100 pamoja na samani zake. Mwaka ujao wa fedha 2022/2023 Halmashauri imetenga jumla ya shilingi Millon 30 kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa shule hii.

Kwa taarifa hii si kweli kuwa katika shule hii wanafunzi wenye mahitaji Maalumu wananyanyaswa na kunyimwa stahiki zao za kila siku bali mazingira rafiki, malezi ya karibu, uungwana pamoja na haki za binadamu huzigatiwa ili kuleta ustawi mzuri wa wanafunzi.

Noah Kibona

Afisa Habari na Mawasiliano

Kny Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya Rungwe

